


# Khilafah

NDIO SULUHISHO

TOLEO NO. 59

RAMADHANI 1440 HIJRI ( MEI 2019 MILADI ) Bei: Tsh 200/- Ksh 5/- Ush 150/-

## RAMADHANI IBADA YA UKOMBOZI

Lengo la Ramadhani ni kuwa tuwe wachamungu. Hii inamaanisha kuwa Waislamu tutakapo itikia wito wa funga ya Ramadhani kwa ukomo wa uelewa wetu katika taratibu za funga na katika utekelezaji wake, bila shaka kwa kiwango fulani tunapata uchajimungu.

Katika kukimbilia fadhila nyingi za mwezi huu, Muislamu hujikurubisha zaidi kwa Allah Ta'ala ili alipwe yalioahidiwa na kupata radhi zake Ta'ala. Mtume saaw amesema:
"Mwezi wenye baraka umekujieni. Allah amefanya funga katika mwezi huo ni wajibu juu yenu. Katika mwezi huo, milango ya Pepo hufunguliwa na milango ya moto hufungwa, na mashetani hufungwa (hutiwa minyororo). Kuna usiku (ndani ya mwezi huu) ambao ni bora kuliko miezi elfu. Yeyote anayenyimwa kheri zake basi amenyimwa kikweli."(Ahmad, an-Nisai, na al-Baihaqi).
Amesema vile vile SAAW: "Funga ni ngao ambayo mja hujikinga kutokana na moto." (Ahmad).
Kwa fadhila na malipo makubwa kama haya Muislamu huwa tayari kutoa muhanga muda wake, juhudi yake na mali yake kwa lengo la kujitakasa zaidi na kwa kutaraji malipo makubwa zaidi ambayo hayapatikani katika miezi mengine. Muumini hupata furaha na kuihisi kuwa hio ndio furaha ya kweli, na sio ile tu ya kushibisha mahitaji yake ya kibaoljia na matamanio yake ya kijinsia ambayo hujizuwia nayo katika mchana wa Ramadhani, huku akiwa radhi na katika kuitikia mwito wa Mola wake.
Ndani ya mwezi huu Muumini hukuza nafsiya yake na kujengeka sehemu yake ya kiroho kwa kufanya ibada mbalimbali kwa ajili ya Allah Ta'ala aliyeumba, na kujikurubisha kwake kwa kufanya yaliyo mema, na kudumu kujenga kila matendo yake juu ya msingi wa imani kwa Allah (swt), huku akiahidiwa na Mola wake Ta'ala:
التَّائِبُونَ الْعَابِدُونَ الْحَامِدُونَ السَّائِحُونَ الرَّاكِعُونَ السَّاجِدُونَ الآمِرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَالنَّاهُونَ عَنْ الْمُنكَرِ وَالْحَافِظُونَ لِحُدُودِ اللَّهِ وَبَشِّرْ الْمُؤْمِنِينَ (التوبة: 112
(*Hao walio ahidiwa bishara njema na kufuzu ni hawa): Wanaotubia, wanaofanya ibada (kwa juhudi kubwa), wanaomshukuru (Allah), wanaofunga, wanaorukuu na kusujudu, wanaoamrisha mema na kukataza mabaya, na wanaohifadhi mipaka ya Allah. Basi wape bishara njema waumini.* (TMQ 9:112)
Muumini huyu huzidisha twaa yake kwa Allah SW katika mwezi huu katika kuitilia nguvu




nafsiya yake na kumpelekea kusonga mbele kuelekea kwenye ubora na utukufu. Atajenga uwezo wa kuyatawala maisha yake kwa mujibu wa vipimo vya 'halali' na 'haramu', kuitafuta kheri kutokana na bidii yake, kufungamana na ibada ya swala na ibada nyengine ikiwemo kuwa shujaa katika kubeba da'wah kwa bidii kubwa. Yote hayo ni kwa ajili ya kupata darja ya pepo ya wafungaji kama alivyosema Mtume SAAW :
*Yule aliye miongoni mwa wenye kufunga ataitwa katika mlango wa funga, mlango wa Raiyan* …" (Bukhari). **(inaendelea Uk. 2 )**

## RAMADHANI: KIPAMBANUZI CHA KIMFUMO

Alhamdulillah tupo katika mwezi mtukufu wa Ramadhani, ni masiku adhimu kwa binadamu wote na haswa Waislamu. Ni mwezi ambao hudhihirisha utu wa mtu kiasili. Kiasili binadamu ni kiumbe mwana jamii (social creature) ambaye huishi na kutekeleza maisha yake kwa kutegemeana na viumbe wengine, akiwemo binadamu mwenzake. Kutegemeana huku kwapasa kufahamike vyema kwa binadamu ambaye ndie kiumbe pekee mwenye akili na utashi ili kuratibu mahusiano yao wenyewe na pia mahusiano yao na viumbe wengine. Kuipuuza au kuidogosha asili hii ni chanzo msingi cha matatizo yote duniani ikiwemo yanayochangia uwepo wa mabadiliko ya tabia nchi (climate change) ambayo hujiri kwa kukosekana kwa ufahamu sahihi juu ya mahusiano haya.Ili kuyafahamu mahusiano haya ndipo mfumo wa Kiislamu ukamjenga




mwanaadamu katika akili inayohisi na kuguswa na hali za wengine. Ibada ya Swaumu ya Ramadhani ni nyenzo msingi kwa mafunzo haya, hususan mahusiano mema baina ya wanaadamu. Kufunga swaumu ya Ramadhani ni kujizuia kufanya mambo ya halali kwa muda maalumu. Kiasili mambo yaliyo haramu, ni haramu muda wote, sio kwa Ramadhani tu. Hivyo, katika mfungo huu Waislamu pamoja na kuwa na uwezo na mambo hayo ya halali, huacha vyakula na vinywaji vyao katika mchana, hujitenga katika jimai na wenza wao kwa mchana na huzidisha matendo mema kwa kutaraji malipo ya thawabu yasioshikika kama kitu cha kimada (intangible benefits). Pia hujipinda kwa toba baada ya kuyatathmini maisha yao na kukiri makosa yao.

Mtu kushinda na njaa kwa khiari japokuwa ana uwezo wa kula na kunywa anachotaka na anapotaka, ni ukumbusho kutoka kwa Allah SW kwa wanaadamu juu ya neema walizonazo ambazo baadhi ya wenzao hawana, ikiwemo chakula. Walionacho huoneshwa uchungu wa njaa na kiu ili wazihisi dhiki na tabu **Uk.4**

# RAMADHANI BEGA KWA BEGA NA MFUMO

Moja katika fadhila kubwa ya mwezi mtukufu wa Ramadhani ni kupatikana ndani yake suala la kuteremshwa Quran, ambayo ni muongozo wa watu, zama na katika kila kipengee cha maisha ya wanadamu.

Allah Taala anasema:

شَهْرُ رَمَضَانَ الَّذِي أُنزِلَ فِيهِ الْقُرْآنُ هُدًى لِلنَّاسِ وَبَيِّنَاتٍ مِنَ الْهُدَى وَالْفُرْقَانِ

*"Ni mwezi wa Ramadhani ndio ambao imeteremshwa humo Qur'an kuwa ni uongofu kwa watu, na hoja zilizo wazi za uwongofu na upambanuzi"*
*(TMQ 2:185)*

Hapa aya kwa muktadha wa nafasi ya Quran imetaja mabo mawili makubwa: Kwanza Quran ni muongozo, ubainifu na kipambanuzi. Pili, muongozo huo umelengwa kwa watu wote, kuna haja ya kujiuliza swali. Vipi Quran itakuwa muongozo kwa kafiri ambaye haiamini, haibebi wala haswali, hafanyi ibada ya Hijja wala hafungi? Inamuongozaje?

Qur'an itakuwa ikimuongoza kafiri kwa khiyari au kwa nguvu katika maisha yake katika upande wa kiutawala kuanzia uchumi, siasa, jamii, elimu nk. na sio katika upande wa ibdaat. Kwani makafiri licha ya kuwa hawalazimishwi kuwa Waislamu,
lakini hutawaliwa juu yao na sheria za Kiislamu katika maisha yao ya kila siku chini ya Dola. Dola ya Kiislamu (Khilafah) ina wajibu kuwatawalia makafri wote kwa sheria za Kiislamu isipokuwa zile ambazo Uislamu umekuja kuzivua. Kama vile sheria za swala, swaum, hijja nk. Kwani ibada hizi kutekeleza kwake sharti msingi kwa mtekelezaji awe na imani ya Kiislamu, na wao makafiri hawana imani hiyo.

Hivi ndivyo alivyofanya Mtume (SAAW) katika kuamiliana na makafiri 'dhimmiy' na ndivyo vivyo hivyo wanavyofanya makafiri mabepari leo kuwalazimisha Waislamu kufuata sheria zao za maisha na kutubakishia mfumo wetu katika mambo ya kiroho tu kama funga, hijja, swala, ushauri nasaha katika masuala ya ndoa na mirathi (ukadhi) nk.
Mfumo wa ubepari unayafanya haya, kwa kuwa hii ni moja katika sifa muhimu na ya lazima ya mfumo wowote. Sifa ya kulazimisha watu wote kuwa chini ya sheria na sera za mfumo unaotawala.
Kwa kuwa Quran imeteremshwa katika mwezi huu wa Ramadhani ikiwa ni muongozo wa maisha wa wanadamu wote, maana yake ni wazi imekuja kutangaza kuwa Uislamu ni mfumo kamili wa maisha

Tamko 'mfumo wa maisha' ni mwelekeo fulani rasmi wa kimaisha unaotokana na itikadi maalumu, na itikadi hiyo huzaa nidhamu mbalimbali za masuluhisho katika nyanja za elimu, siasa, jamii, uchumi, utawala, ibada nk. kwa ajili ya kutekelezwa chini ya utawala. Mfumo huo hutabikishwa kwa walioamini, na pia hutabikishwa hata kwa wasiouamini.

Ikiwa imani/dini imekosa nidhamu za maisha kutoka ndani ya imani hiyo. Dini hiyo huwa si mfumo wa maisha, bali inabakia kuwa dini tu. Kama zilivyo imani/dini za ukristo, uyahudi, ubaniyani,ubudha nk.ambazo hujihusisha na fungamano la mtu na Mola wake tu bila ya kuwa na masuluhisho yoyote katika maisha ya kila siku.

Kwa bahati mbaya kuna wanaotumia tamko hili la mfumo wa maisha wa Kiislamu, kwa maana finyu na isiyokamilika kinyume na inavyotakikana kufahamika na kulinganiwa kwa mujibu wa Uislamu.

Badhi huhubiri Uislamu kuwa ni mfumo kamili wa maisha, lakini mifano wanayoitoa bado haifikii maana halisi na pana ya tamko la mfumo wa maisha. Wengi huishia kutoa mifano ya namna ya Uislamu unavyofundisha kula, kunywa, kwenda haja, kuvaa nguo, kufanya jimai na dua kadhaa wa kadhaa. Kwa ufahamu wao huo wao huona hii ndio maana kamili ya kuwa Uislamu ni mfumo kamili wa maisha ya Muislamu tangu anapotoka usingizini, anaposhinda mchana mpaka anaporudi tena usiku kulala.

Pamoja na ukweli kwamba hayo ni sehemu katika mfumo wa Kiislamu. Lakini bado haijakamillika maana halisi na pana ya tamko 'mfumo' kwa upana wake kwa kuwa hayakuhusisha sehemu muhimu ya uchumi, siasa za ndani, siasa za nje, vita, mahusiano ya mikataba na nchi za kikafiri, fedha ya nchi (sarafu) nk.

Huu ndio ufahamu wa nafasi ya muongozo na mfumo wake wa Kiislamu. Ndani ya mwezi huu mtukufu wa Ramadhani ulioteremshwa Quran tuna umuhimu mkubwa kufafanua kwa kina kwa Ummah, ili uweze kushiriki kikamilifu kuurejesha tena maisha ya Kiislamu kwa kurejesha tena utawala wa Khilafah Rashidah.

*(kutoka Uk. 1)*

Swaumu katika mwezi huu humjenga Muumini kuwa mwenye subra, mkarimu, mnyenyekevu, mwenye huruma, mwenye moyo uliyostawi uchaji Mungu, na huku viungo vyake vikikimbilia wema badala ya maovu yanayomkasirisha Muumba wake. Akiwa mwenye moyo laini, ulio mtulivu na tamaa ya rehma za Mola wake, hukimbilia yale yenye kumridhisha Allah pekee na kuwacha maovu yenye kumkasirisha Allah SW. Huwa pamoja na Allah SW usiku na mchana akifunga mchana wake na kuswali usiku wake, kuwa tayari kumuitikia Mola wake katika hali zote
Muumini huyu hatomalizia tu kujitakasa nafsi kwa ibada khaswa kama swala, swadaka nk. Bali husonga mbele zaidi peke kwa kuwa mletaji wa ukombozi wa kikweli katika ulimwengu huu uliojaa dhulma, ufisadi na kila aina ya uovu. Kwa kupitia ibada hii ya funga na muitikio wake wa kikweli kwa Allah SW katika matendo yake kumemfanya moyo wake na nafsi yake kuwa tayari kwa mwito wa ukombozi unaotokana pia na Mola wake Mtukufu, Mwenye nguvu na Aliye Mkuu, na Ambae kupitia kwake ndiko kwenye ushindi. Ndipo ikashuhudiwa katika historia ya Uislamu ndani ya mwezi huu kupatikana ushindi muhimu huku Waislamu wakiwa katika ibada ya swaum. Miongoni mwao ni Vita vya Badri, Fathu Makkah, Fathi ya Andalusia (Spain na Ureno) ushindi wa Salahuddin kwa Makruseda, ushindi katika Vita vya Ain Jaluut nk.

**Habib Abdullah**

**TAHARIRI**

Wakati tukiwa ndani ya mwezi mtukufu wa Ramadhani, licha ya kujifunga na ibada mbali mbali ni lazima pia ikite katika ufahamu wetu juu ya fungamano kubwa la mwezi wa Ramadhani na kitabu kitukufu cha Quran.
Mwezi huu ndio ambao Allah Taala kauteua kuteremsha kitabu ambacho ni muongozo kwa mambo yote na wanadamu wote.
Kwa bahati mbaya leo ni karibu miaka .. hatuishi chini ya kivuli cha dola yetu tukufu ya Khilafah, kwa maneno mengine muongozo wetu haufanyi kazi kwa upana wake licha ya kuwa mambo ya kibinafsi Alhamdullilah tunaendelea nayo. Kukosekana utawala wa kuitabikisha muongozo ni hasara sio tu kwa Waislamu bali kwa wanadamu kwa jumla. Ni wajibu kufanya kazi usiku na mchana ili kurejesha utawala utakaoutawalisha muongozo huu wa kama lilivyo lengo lake. Tunawatakia Ramadhani njema.

**MHARIRI**
**05 Ramadhan 1440AH/ 11 Mei 2019**

**gazetikhilafah@gmail.com**

**http://hizb.or.tz/**
https://twitter.com/Hizb_tanzania
**https://www.facebook.com/Hizb-ut-Tahrir-Tanzania**

## Makala ya Wanawake




Mwezi wa Ramadhani ni mwezi wa furaha na majonzi kwa munasaba wa kumbukumbu ya Bi. Khadija ra. Mama wa Waumini na mke wa mwanzo wa Mtume wetu SAAW.

Katika mwezi huu mtukufu ndipo Mama huyu mtukufu ra. alipoikubali nuru ya Uislamu na kuupata utukufu wa kuwa mwanamke na miongoni mwa wa mwanzo kuikubali risala ya Uislamu Aidha, mwezi huu wa Ramadhani ndio mwezi alipofariki mama huyu mtukufu na kumuacha Mtume SAAW katika majonzi, huzuni na simanzi isiyomithilika hususan kwa kuwa kifo chake kilipishana kwa muda mfupi wa miezi miwili tu na kifo cha ammi yake Mtume SAAW.

Ni umakini na unyenyekevu wa mama huyu ndio uliyompelekea kufikia hatua ya kuikubali nuru ya Uislamu kinyume na walio wengi katika jamii ya Makka. Kwa sababu lau tukisema sababu ya kusilimu kwake ni kuwa kwake mke wa Mtume SAAW, hilo sio sawa, kwa kuwa wako wanawake kadhaa katika historia waliokuwa wake za Mitume As. ambao nuru ya tawhid ilikuwa inaangaza ndani ya majumba yao, lakini kamwe wao hawakuikubali. Mfano, ni mke wa Nabii Nuh As. na Nabii Lut As.

Fadhila, utukufu, hadhi na nyota ya Bi Khadija ra. ilidhihirika mapema katika maisha yake kabla hata ya kuanza kuamiliana na Mtume SAAW. Kama alivyokua Mtume SAAW kabla ya Utume, jamii ya Makka ilimpa cheo cha Aswadik ul-amiin (Mkweli Muaminifu) Bi. Khadija nae katika jamii hiyo alikuwa akiitwa Atwahirah (aliyetakasika). Alikuwa bibi huyu ana khulka njema na murua wa kupigiwa mfano katika jamii ya Makka. Licha ya umri wake kusonga, na kuwa mjane kwa kufiliwa na waume wawili, bado utukufu na haiba yake ndani ya jamii ya Makka ilikua juu, kiasi cha wanaume mbalimbali kumkabili kumposa, lakini alihisi hawakuwa chaguo muwafaka.
Bi Khadija alibakia katika hali hiyo mpaka alipoamiliana na Mtume SAAW katika biashara zake ndipo alipokuja kugundua haiba njema na karama ya Mtume SAAW iliyoambatana na barka katika biashara na uaminifu wa darja ya juu, Bi Khadija akaona Mtume SAAW ni mtu muwafaka wa kuwa mume wake, licha ya kuwa Mtume SAAW alikuwa mtu mwenye kipato cha chini. Baada ya Bi Khadija kupata taarifa njema kuhusu Mtume SAAW kutoka kwa mfanyakazi wake Masara aliyeambatana na Mtume SAAW katika masafara wa kibiashara katika nchi Al-Sham alivutika sana na Mtume SAAW na haraka kumtuma shoga yake Bi Nafisa kumshauri Mtume SAAW juu ya suala la ndoa .

Ndoa ya Mtume SAAW na Bi Khadija ikawa ufunguo wa kila kheri kwa pande zote mbili. Bi Khadija aliyekulia katika familia yenye mwanazuoni wa Ahlul Ktaab Warqa bin Naufal ambae aliwapasha khabari ya kuja Mtume, kwa haraka bila aliukubali Utume wa Mtume SAAW.
Kuanzia hapo na katika miaka 25 ya ndoa yao, Bi. khadija akawa msaada, faraja, maliwazo, mfadhili na muhimili mkubwa wa kujitolea hali na mali yake kwa ajili ya Mtume SAAW na Uislamu kwa jumla. Akamuunga mkono Mtume SAAW hususan katika kipindi kigumu cha miaka kumi ya ulinganizi bila ya kurudi nyuma wala kutetereka. Akapata hadhi ya kuwa mama wa mwanzo wa Waumini, akawa mama wa kizazi chema. Mtume wetu SAAW anasema :
.. ***Aliniamini mimi , wakati watu wakinikataa, akaniswadikisha wakati watu wakinikadhibisha, akanishirikisha katika mali yake wakati wengine watu wakininyima, na Mwenyezi Mungu akaniruzuku watoto nae ……***
Huyu ndio Bi Khadija ambae katika mwezi huu tunamkumbuka. Ni muhimu kwa wanawake wa Kiislamu kufuata nyayo zake ili wafanikiwe duniani na akhera. **Ummu Ammar**

*Ukumbi wa Fiqhi*

## UFAFANUZI KUHUSU DAKU

Fadhila za kula daku (suhoor) ni nyingi sana. Anas bin Maalik (ra) amesema, amesema Mtume SAAW "kuleni daku kwani katika daku kuna baraka" Al-Bukhaari (1923). Ibn Umar (ra) pia amesema, amesema Mtume ﷺ"Hakika Allah SW na Malaika wake huwaombea walaji wa daku"Ibn Hibbaan (3468). Kutoka kwa Abu Hurairah (ra), amesema Mtume " ﷺbaraka iliyoje kula daku kwa tende(Tamr). Pia Abbdullah ibn 'Amru (ra), amesema Mtume ﷺ "kuleni daku hata kama ni kwa funda la maji"

Hivyo, daku ni baraka ambayo Allah SW anawapa Waumini. Endapo Waumini watakula daku basi wataombewa dua na Allah SW na Malaika.
Ubora wa daku ni kula tende mbichi (ratwab),tende kavu(tamr) au maji. Hizo ndio fadhila za daku, lau kungekuwa hakuna fadhila zozote katika kula daku, basi dua ya Allah SW na malaika pekee yatosha kutufanya tule daku.

Hukm ya kisheria ya kula daku (As-Suhoor) wamesema An-Nawawi na Ibn ul-Mundhir ni Mustahabb kwa Ijmaa na siyo faradhi.

Katika Al-Mughni Ibn Qudaamah anasema: 'kuhusu kula daku kuwa ni Mustahab, hajui rai nyingine tofauti na hiyo. Huu ndio ukweli wake, na hadithi za fadhila za kula daku zinaonesha kuwa ni Mustahab na si faradhi.

Ni rai ya maimamu wanne na wanachuoni wengine wakubwa kuwa, muda wa mwisho wa kula daku ni mwanzo wa alfajir au mpaka atakapoadhini muadhini wa pili (adhana ya kuswalia Swala ya Fajr). Rai yenye nguvu ni ile ya maimamu na wengi miongoni mwa maulamaa kuwa kula, kunywa, na kujimai ni mpaka utakapokuwa na hakika ya kuingia fajr.

Allah SW anasema:
"…na kunyweni na kuleni hata utakapoweza kutofautisha uzi mweupe na mweusi.." (Al-Baqarah :187)
Sahl Ibn Sa'd (ra) anasema iliposhuka aya "…na kuleni na kunyweni hata mutakapoweza kutofautika kwenu uzi mweupe kwa mweusi.." ilikuwa watu wanafunga nyuzi nyeusi na nyeupe miguuni mpaka watakapoweza kutofautisha nyuzi hizo. Liliposhuka tamko 'min al-fajr', hapo wakafahamu kuwa ilimaanisha usiku na mchana. (Bukhaari na Muslim)

Aisha (ra) alisema: "Mtume SAW alisema, kuleni na kunyweni mpaka atakapoadhini Ibn Ummu Makhtoom...na hakuwa akiadhini(Ibn Makhtoom)ila ilipoingia alfajir"(Bukhaar )

Kutokana na dalili hizo na nyingine, tunajifunza kuwa Aya ya Allah SW kuhusu daku inakusudia muda wake ni mpaka itakaoingia alfajir na kutoweka usiku.

Sunnah ya Mtume SAAW ni kuchelewesha kula daku mpaka unapokaribia muda wa fajr. Walikuwa masahaba wakichelewa kula daku ili kupata fadhila zake. Na hawakuwa wakila daku katikati ya usiku au saa moja au masaa mawili kabla ya adhana ya swala ya fajr, bali walichelewesha mpaka muda karibu na adhana ya swala ya fajr.

**Imefasiriwa na Said Bitomwa**




## ‘RAMADHANI NA MUONGOZO WA QURAN’

Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari Masoud Msellem (katikati) na Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano wa Hizb ut Tahrir Tanzania Sheikh Mussa Kileo (mwenye miwani)wakiwa katika kampeni ya‘Ramadhani na Quran’ katika muhadhara uliofanyika Masjid Islah , Kigogo Dar es Salaam. Kwa maelezo zaidi ya kampeni:

http://hizb.or.tz/2019/05/03/ijue-kampeni-ya-ramadhani-na-muongozo-wa-quran/

**kutoka Uk 1)**

za kushinda na njaa huku wakikodolea macho majokofu (friji) yako yaliosheheni vyakula na vinywaji. Ni kama masikini wanavyoumia huku wakikodolea macho na kuumia pua kwa vyakula vinono vya matajiri, au bidhaa madukani na majumbani. Hivyo basi, kufunga huku ijengeke kwa wafungaji nishati ya kuwasukuma kuwasaidia wengine kwa kile walichojaaliwa na Allah SW. Kujitolea huku ni kwa kutafuta kuridhiwa na Allah SW na sio kwa kupata manufaa mbadala ya kushikika (material benefits).

Kwa masikitiko leo jamii inaishi chini ya mfumo wa kirasilimali/ kibepari ambao huongozwa na siasa ya kidemokrasia (kumtenga Mungu Muumba na maisha ya viumbe). Msingi mkuu wa ubepari ni kujenga kila fikra juu ya faida za kimaada, ambayo hupelekea watu kuwa wabinafsi, kutojali nafasi ya Mungu Muumba (Qadhaa) katika kufanikiwa na kufeli katika juhudi za mtu. Huchukuliwa kuwa kila aliyefanikiwa ni kutokana na akili yake, na aliyeshindwa ni uzembe na kutojituma kwake.

Ubepari umejenga thamani ya mtu ni kutokana na mali anayoimiliki, **asiye** kuwa na kitu/mali hana utu. Fikra hii ikasukuma watu kuchuma kwa kila njia hata iwe ya kudhuru wengine (kama ujambazi, rushwa, utapeli na riba) ili tu kujikusanyia mali. Katika maisha haya, mwenye nacho humsaidia asiye nacho pale tu atakapojihakikishia kukuza kipato chake kimali**.** Ima kwa kulipwa mali moja kwa moja au kupata nafuu ya kisera itakayomuongezea faida katika utafutaji wake.

Ni Uislamu pekee unaotaka mtu kujali shida za mwenzake bila kutaraji malipo kutoka kwake, akiamini mtoaji kwamba ni Muumba pekee ndie Aliyemruzuku hicho alichonacho. Muumba ambae Anaweza kukichukua, akabakia mwanadamu katika hali kama ya asiyenacho kwa muda huo.

Kwa hiyo, utakuta lau jamii itakua chini ya serikali ya Kiislamu (ambayo haipo duniani leo hii) hakutokuwa na watu wanaokula na kusaza kwa kiwango cha kukuta majaa yamejazwa vyakula vilivyowashinda. Wala hutakuta watu wen

enye dhiki ya kukosa

mlo japo mmoja, kwani tatizo lao ni tatizo la wenzao walio na nafuu, hulitatua pamoja kama jamii.

Katika mwezi huu wa Ramadhani hudhihirika athari ya utulivu wa jamii. Kila mmoja anakiri kupungua kwa maasi katika jamii, ikiwemo wizi, ulevi, umalaya nk. Haya ni natija/ matokeo ya maisha ya mfumo wa Kiislamu. Mfumo ambao hauna serikali kwa sasa, lakini yanaleta athari na watu hubadilika kitabia kutokana na nishati ya kiimani na kwa msukumo wa kiutu na hisia za kibinadamu tu, sio kwa nguvu ya dola, polisi wala mahakama kama ilivyo katika jamii hizi za kibepari.

Tunaona wafungaji wa Ramadhani hujiepusha kuwakera wengine ili kuhakikisha kufaulu kwa ibada yao. Hujizuiya kutukana, kugombana, na hata wizi na ujambazi hupungua.Wakati mwingine hata wasiokuwa Waislamu, baadhi ya wenye ufahamu wa kiutu hujiepusha na mambo ambayo ni kero katika jamii ili wasiwakwaze Waislamu wanaofunga.

Utulivu huu wa jamii kwa mwezi wa Ramadhani uibue hisia thabiti na ujenge fikra za hitajio la usimamizi wa ujumla wa Uislamu katika maisha yetu baada ya kujiuliza, iwapo bila ya dola (Khilafah), jeshi wala mahakama jamii inabadilika hivi, jee ukiwepo usimamizi kwa sharia kamili za Allah SW na muongozo wa Mtume SAW, utulivu na ustawi wa jamii utakuwa mkubwa kwa kiasi gani ?

Jambo hili pia ni changamoto kwa wasiokuwa Waislamu kwa kuibua mjadala juu ya mfumo wa kibepari na nidhamu yake ya kidemokrasia, kwani pamoja na kuwa na dola, majeshi, mahkama na vyombo vyengine vya dola bado hali ya kukosekana amani na utulivu inazidi kuzorota kila uchao. Aidha, hali hii ilete msukumo kwa jamii nzima kuona umuhimu wa siku zote kuwa ‘masiku ya mwezi mtukufu wa Ramadhani’, kushikamana na maadili mema bila shuruti.

**Abu Nuthutaq**